**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME**

S. L. P 16,
HEDARU-SAME.
14/12/2021.

**Shule ya Sekondari Chauka** **Simu: +255 712 857 424**

Jina la Mwanafunzi__________________________ .

## YAH: KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHAUKA KIDATO CHA KWANZA MWAKA WA MASOMO 2021.

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka wa masomo 2021. Mhula wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021**, unashauriwa kuripoti siku hiyo kwa usajili.

**Mambo Muhimu ya Kuzingatia.**

**1.0 Sare ya Shule**

**Wavulana**

1.1 Suruali mbili (02) moja rangi ya **Kijivu** itakayovaliwa siku ya jumatatu, jumanne na jumatano na ya pili ni rangi ya **Khaki** itakayovaliwa siku ya alhamisi na ijumaa.

1.2 Mashati mawili (02) meupe ya tetron (Tomato) ya mikono mifupi

1.3 Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili (02) vyenye matundu sita ya kufunga kwa kamba na kisigino kifupi.

1.4 Soksi nyeusi fupi jozi mbili (02)

1.5 Masweta (02) yafanane na rangi za suruali ambazo ni kijivu na khaki.

**Wasichana**

1.6 Sketi ndefu mbili (02) moja rangi ya **Kijivu** itakayovaliwa siku za jumatatu, jumanne na jumatano na ya pili ni rangi ya **Khaki** itakayovaliwa siku ya alhamisi na ijumaa

1.7 Mashati mawili meupe ya tetron (Tomato) mikono mifupi. (kwa wanaovaa hijabu mashati yawe ya mikono mirefu)

1.8 Soksi ndefu nyeupe jozi mbili (02)

1.9 Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili (02) vinavyofunuka miguu vyenye kisigino kifupi na vya matundu sita ya kufunga kwa kamba.

1.10 Masweta (02) yafanane na rangi za sketi ambazo ni kijivu na light khaki.

1.11 Kwa wanaovaa **Hijabu** iwe ndefu nyeupe ya heshima, isiyobana na isiwe na urembo wowote.

**Muundo wa Mashono ya Sare.**

**(a) Suruali:** Ziwe pana (sio modal) na ziwe na marinda matatu mbele. Ziwe na upana wa kutosha kwa chini na ziwe na "turn up" .

**(b) Sketi :** Ziwe na marinda (rinda box) pamoja na ribbon nyeupe mistari miwili upande wa mkono wa kulia. Zisiwe na mkanda mpana (kantangaze) ziwe ndefu na zisizobana.

**2.0 Vifaa vya Taluma na Mahitaji Mengine**

2.1 Madaftari makubwa 11 (Counter Books Quire 3), kalamu (02) za wino nyeusi/bluu, penseli, ufutio, mkebe (mathematical set), rula, begi imara na kamusi (dictionary) aina ya oxford ya lugha ya kingereza kwa kingereza.

**N.B.** Daftari (counter books) zote ziwe zimejaladiwa kwa karatasi ya kaki

2.2 Sahani na kikombe cha nusu lita (rangi ya chungwa (orange), na kijiko kwa ajili ya chakula na uji.

**3.0 Vifaa vya Michezo kwa Wavulana na Wasichana Wote**

3.1 Raba za michezo rangi nyeupe

3.2 Bukta na T-shirt za blue (Jezi).

3.3 Truck suit ya rangi ya dark blue, yenye mistari meupe pembezoni.

3.4 Soksi ndefu za michezo rangi ya bluu.

**4.0 Vifaa vya Usafi**

4.1 Wavulana wote kila mmoja alete jembe **jipya** na mpini wake na fagio moja (01) la chelewa

4.2 Wasichana wote kila mmoja alete ndoo mpya ya lita 10 na kwanja moja (01)

**5.0 Sheria na Kanuni za Shule.**

Shule inaongozwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha tunazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

5.1 Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenyewe na jamii kwa ujumla ni muhimu.

5.2 Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

5.3 Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya juu.

5.4 Kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako hapa shuleni.

5.5 Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule wakati wote. Mwanafunzi haruhusiwi kufuga nywele ndefu, kusuka au kubadilisha nywele kwa kutumia madawa ama vinginevyo. Nywele zisizidi urefu wa 5mm (millimeta 5 tu)

5.6 Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

5.7 Kuzingatia kikamilifu ratiba ya shule wakati wote.

5.8 Kuheshimu kengele pindi tu inaposikika

5.9 Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

**6.0 Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Mwanafunzi Kufukuzwa Shule**

6.1 Wizi

6.2 Uasherati na Ushoga

6.3 Ubakaji na makoa mengine ya jinai

6.4 Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k

7.5 Kupigana au kupiga.

7.6 Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

7.7 Kudharau Bendera ya Taifa.

7.8 Kuoa au kuolewa.

7.9 Kupata mimba au kuharibu (kutoa) mimba ndani na nje ya shule.

7.10 Kugoma kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa Shule.

7.11 Kukataa adhabu halali kwa makusudi.

7.12 Mwanafunzi kuwa (kumiliki) na simu ya mkononi.

**8.0 Mambo Mengine Muhimu Yanayopaswa Kukamilishwa na Kuwasilishwa Shuleni na Mwanafunzi**

8.1 Fomu ya uchunguzi wa afya "Medical Examination Form" iliyoambatanishwa ijazwe baada ya kupimwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali au kituo cha Afya. Ikabidhiwe kwa Mkuu wa shule mara utakapo ripoti shuleni.

**NB**: Mzazi kama mwanao ana tatizo lolote la kiafya usisite kuliweka wazi

ili na sisi tumwekee mazingira mazuri ya kumlea.

8.2 Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi .

**9.0 Tafadhali Soma kwa Makini Maelezo/Maagizo Haya na Kuyatekeleza Kikamilifu.**

Mwanafunzi hatopokelewa shuleni ikiwa hakutimiza mojawapo ya maagizo yote tuliyokubaliana hapo juu.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI CHAUKA.

Wenu katika elimu na malezi,

…………………………

FATUMA .A. GORRAH.

**MKUU WA SHULE**

**HALMASHAURI YA WILIYA YA SAME**
**SHULE YA SEKONDARI CHAUKA**
**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

---

**A: JAZA KIKAMILIFU NA KWA USAHIHI**

1. Jina kamili la mwanafunzi ___________________________Me ( ) K e ( )Weka **(√)** panapostahili.
2. Tarehe na mwaka wa kuzaliwa_____________________________________.
3. Shule ya Msingi uliokotoka _______________________________________.
4. Jina kamili la mzazi/mlezi _________________________________________.
5. Anuani ya mzazi/ mlezi ___________________________________________.

**B: WEKA (√) NA TOA MAELEZO PANAPOSTAHILI.**

6. Yatima, NDIO ( ) HAPANA ( ), mzazi mlezi mmoja ( ) wawili ( ) Eleza kuwa ni baba/mama au wote wawili ______________________________________.
7. Anaye husika kukusomesha :
   Jina kamili _____________________________Uhusiano/undugu _________________.
   Kazi yake ______________________________.Sekta/Taasisi itaje__________________.

**C: TAMKO LA MWANAFUNZI**

Mimi _______________________________.ninakubali kuchaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Chauka mwaka 2020

Ninaahidi kuwa nitajitahidi kwa uwezo wangu wote na kutii sheria zote za shule. Sitaleta usumbufu wa aina yoyote kwa mzazi/mlezi wala uongozi wa shule.

Sahihi ya mwanafunzi _____________________Tarehe _____________________.

**D: TAMKO LA MZAZI/MLEZI**

Mimi ____________________________mzazi/mlezi wa mwanafunzi______________________.

Ninaahidi kugharamia mahitaji yote muhimu ya shule na sitomkosesha haki yake na elimu na pia sitaleta usumbufu wa aina yoyote kwa uonogozi wa`shule.

Sahihi ya mzazi/mlezi ___________________ Tarehe _______________________.

**NB**: Tafadhali uje na form hii ikiwa imejazwa kikamilifu.

Nakutakia utelezaji mwema.

………………
FATUMA .A. GORRAH
**MKUU WA SHULE.**

# SHULE YA SEKONDARI CHAUKA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA`MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME**

Kumb. Na: Simu +255712857424

Chauka Sekondari,
S. L. P 16,
Hedaru-Same.

**14/12/2020.**

Mganga Mkuu (W)
Kituo cha Afya
_______________,
_______________.

**YAH: MWANAFUNZI KIDATO CHA I MWAKA 2021**

Rejea somo tajwa hapo juu:
Ninaomba utusaidie kumfanyia uchunguzi mtajwa hapo juu kisha utujazie sehemu husika hapo chini. Natanguliza Shukrani.

……………………………
Mkuu wa Shule-CSS.

Tafadhali tumia alama **(√ )** sehemu ya Ndio au (**X**) sehemu ya Hapana.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. | Kifafa | Ndio | ( ) | Hapana | ( ) |
| 02. | Moyo | Ndio | ( ) | Hapana | ( ) |
| 03. | Ukosefu wa damu (Anemia/sickle sell) | Ndio | ( ) | Hapana | ( ) |
| 04. | Pumu | Ndio | ( ) | Hapana | ( ) |
| 05. | Kisukari | Ndio | ( ) | Hapana | ( ) |
| 06. | Vidonda vya tumbo | Ndio | ( ) | Hapana | ( ) |
| 07. | Kichocho | Ndio | ( ) | Hapana | ( ) |
| 08. | Malaria sugu | Ndio | ( ) | Hapana | ( ) |
| 09. | Magonjwa ya zinaa | Ndio | ( ) | Hapana | ( ) |
| 10. | Ujauzito | Ndio | ( ) | Hapana | ( ) |
| 11. | Je ana dosara nyingine yoyote ya kiafya?. **ITAJE** (Mfano: Macho, masikio au ulemavu mwingine)………………………………………………………………….. ……………………………………………………………………………….. ……………………………………………………………………………….. | | | | |

……………………………
Jina ………………………..

Muhuri